

WHAT 0757478868 RATIONALIZED 2026 T123 SCHEME OF WORK LESSON

PLANS, RECORD OF WORK, LATEST EXAM SERIES TERM 3 JESMA,

COMPASS , SIGNAL ETC 2026 GRADE 8 RATIONALISED AGRICULTURE AND NUTRITION LESSON PLANS - TERM 3

2026 GRADE 8 RATIONALISED KISWAHILI LESSON PLANS - TERM 3

WIKI YA 1: Mada Kuu - Magonjwa Yasiyoambukizwa

Somo la 1

SHU LE	ENEO LA SOMO	Gre di	IDA DI	MUD A
	Kiswahili	8		

MADA KUU: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA **MADA NDOGO:** Kusikiliza kwa Makini **MATOKEA MAALUM YANAYOTARAJIWA:** Kufikia mwisho wa somo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza habari katika matini ya kusikiliza.
- Kuwasilisha hoja muhimu katika habari aliyosikiliza kwa kufuata mpangilio ufaao.
- Kujenga mazoea ya kufurahia kusikiliza vifungu ili kuimarisha uwezo wa kusikiliza.

SWALI DADISI: Je, kwa nini ni muhimu kuwa na mpangilio ufaao wa hoja kutoka habari uliyosikiliza?

VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA KUFUNDISHIA:

- Akili Pevu Kiswahili Gredi ya 8, ukurasa 138
- Kifaa cha kidijitali (k.m., redio, simu)
- Chati ya msamiati

MPANGILIO WA SOMO: Wanafunzi watafanya kazi mmoja-mmoja, wawili-wawili, na kisha kama darasa zima.

UTANGULIZI Mwalimu atawauliza wanafunzi wataje baadhi ya magonjwa wasiyoambukizwa wanayoyafahamu. Mjadala huu utaongoza kwenye mada ya siku na umuhimu wa kusikiliza kwa makini ili kupata habari sahihi.

UENDESHAJI WA SOMO Wanafunzi wanaongozwa:

- **HATUA YA 1:** Kusikiliza kwa makini habari kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa ikisomwa na mwalimu au kutoka kwa kifaa cha kidijitali.
- **HATUA YA 2:** Mmoja-mmoja, kutambua na kuandika hoja muhimu kutoka kwa matini waliyosikiliza.
- **HATUA YA 3:** Wawili-wawili, kujadili hoja walizoandika na kuzipanga kwa mtiririko unaofaa.
- **HATUA YA 4:** Kueleza maana ya msamiati mpya uliotumika katika matini (k.m., *kisukari, shinikizo la damu, saratani*).

HITIMISHO Mwalimu atatoa muhtasari wa umuhimu wa kutambua na kupanga hoja muhimu kutoka kwa matini ya kusikiliza. Wanafunzi wachache watachaguliwa kueleza hoja muhimu walizozipata kwa maneno yao wenyewe.

MAZOEZI YA ZIADA Wanafunzi wamsomee mzazi au mlezi habari kuhusu suala hili na washirikiane kutambua hoja muhimu.

TAFAKARI KUHUSU

SOMO
.....
.....

Somo la 2

SHU LE	ENEO LA SOMO	Gre di	IDA DI	MUD A
	Kiswahili	8		

MADA KUU: KUSOMA MADA NDOGO: Kusoma kwa Ufasaha **MATOKEA MAALUM YANAYOTARAJIWA:** Kufikia mwisho wa somo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora.
- Kusoma kifungu kwa kasi ifaayo.
- Kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo za mwili.